**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# MKUTANO WA KUMI NA SITA NA KUMI NA SABA

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI NA SABA

***(DAILY SUMMARY RECORD OF PROCEEDINGS)***

**26 NOVEMBA, 2014**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA NA KUMI NA SABA**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI NA SABA**

**(SUMMARY RECORD OF PROCEEDINGS – SEVENTEENTH SITTING)**

**TAREHE 26 NOVEMBA, 2014**

## I. DUA:

Mwenyekiti wa Bunge Mhe. Mussa Azzan Zungu alisoma Dua saa 3.00 asubuhi na Kikao kiliendelea.

MAKATIBU MEZANI:
1. Ndg. Ramadhan Abdallah
2. Ndg. Lawrence Makigi
3. Ndg. Asia Minja

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Amina Mohammed Mwidau aliwasilisha tarifa maalum ya Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu taarifa ya Ukaguzi maalum kuhusiana na miamala iliyofanyika katika akaunti ya ESCROW ya TEGETA pamoja na umiliki wa kampuni ya IPTL.

## III. MASWALI

Maswali yafuatayo yaliulizwa na kujibiwa;

1. OFISI YA WAZIRI MKUU

Swali Na. 205: Mhe. Moses J. Machali [kny: Mhe. Halima Mdee]

Nyongeza: (i) Mhe. Moses J. Machali
(ii) Mhe. Richard M. Ndassa

Swali Na. 206: Mhe. Zainab Matitu Vullu [kny: Mhe. Sylvester F. Koka]

Nyongeza: (i) Mhe. Zainab Matitu Vullu
(ii) Mhe. Maryam Salum Msabaha

Swali Na. 207: Mhe. Mch. Luckson Mwanjale [kny: Mhe. Dkt. Mary M. Mwanjelwa]

Nyongeza: (i) Mhe. Mch. Luckson Mwanjale
(ii) Mhe. Aliko Nikusuma Kibona
(iii) Mhe. David Ernest Silinde

2. WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO

Swali Na. 208: Mhe. Murtaza Ally Mangungu

Nyongeza: (i) Mhe. Murtaza Ally Mangungu
(ii) Mhe. Alphaxard K. N. Lugola
(iii) Mhe. Yussuf Salim Hussein
(iv) Mhe. Hamad Rashid Mohamed

3. WIZARA YA MAJI

Swali Na. 209: Mhe. Rukia Kassim Ahmed

Nyongeza: (i) Mhe. Rukia Kassim Ahmed
(ii) Mhe. Rita Louise Mlaki
(iii) Mhe. Iddi Mohammed Azzan
(iv) Mhe. Muhammad Ibrahim Sanya

Swali Na. 210: Mhe. Dkt. Henry Daffa Shekifu

Nyongeza: (i) Mhe. Dkt. Henry Daffa Shekifu
(ii) Mhe. Suleiman M. N. Suleiman
(iii) Mhe. Stephen Hillaly Ngonyani

4. WIZARA YA NISHATI NA MADINI

Swali Na. 211: Mhe. Diana Mkumbo Chilolo

Nyongeza: (i) Mhe. Diana Mkumbo Chilolo
(ii) Mhe. Josephine Genzabuke
(iii) Mhe. Suzan A. J. Lyimo
(iv) Mhe. Hussein Nassor Amar

(v) Mhe. Mohamed Hamisi Missanga

Swali Na. 212: Mhe. Shaffin Ahmedali Sumar

Nyongeza: (i) Mhe. Shaffin Ahmedali Sumar
(ii) Mhe. Philipo Augustino Mulugo
(iii) Mhe. Moza Abeid Saidy

5. WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA

Swali Na. 213: Mhe. Said Amour Arfi

Nyongeza: (i) Mhe. Said Amour Arfi

Swali Na. 214: Mhe. Modestus Dickson Kilufi

Nyongeza: (i) Mhe. Modestus Dickson Kilufi

6. WIZARA UJENZI

Swali Na. 215: Mhe. Mendrad Lutengano Kigola

Nyongeza: (i) Mhe. Mendrad Lutengano Kigola

7. WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII

Swali Na. 216: Mhe. Zarina Shamte Madabida

Nyongeza: (i) Mhe. Zarina Shamte Madabida

8. WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

Swali Na. 217: Mhe. Mwanakhamis Kassim Said

Nyongeza: (i) Mhe. Mwanakhamis Kassim Said

Swali Na. 218: Mhe. Haroub Mohammed Shamis

Nyongeza: (i) Mhe. Haroub Mohammed Shamis

## IV. MATANGAZO

Wageni mbalimblai walioko kwenye gallery walitambulishwa wakiwemo kutoka ofisi ya CAG na ofisi ya vyama vya Siasa wakiongozwa na Jaji F. Mutungi.

Aidha matangazo mbalimbali ya Kamati yalitangazwa.

**MIONGOZO YA SPIKA**

1. Mhe. Suleiman Nchambi Suleiman aliomba mwongozo kuhusu Mahakama kuzuia mjadla wa ESCROW na kwamba suala hili limepelekwa na Wakili wa CHADEMA na akaomba naye ajadiliwe na kwamba CCM ndiyo inataka mjadala na sio CHADEMA waliopeleka.

2. Mhe. Tundu Anthipas Lissu alielekeza kwamba Wakili wa PAP/ESCROW ni Gabriel Mnyele Mpanda na ni Mwana CCM na sio CHADEMA kama alivyosema Mhe. Suleiman Nchambi. Pia alieleza kwamba suala la Mahakama kuzuia mjadala halijawahi kutokea toka 1922 na ni kuingilia uhuru, na ibra 4 na 100 ya Katiba zimekiukwa. Bunge liendeleee na mjadala.

3. Mhe. Christopher Ole-Sendeka alisema Ibara ya 100 ya Katiba imelipa Bunge Mamlaka ya kujadili bila kuingiliwa hivyo wabunge waendelee na mjadala.

4. Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa alitoa ufafanuzi kwamba Spika alishatoa Rulling Bunge halitakiwi kuwa na wasiwasi liendelee na mjadala.

5. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga alisema Spika kwa siku iliyopita alishasema waendelee kujadili na wasiendelee kupoteza muda.

6. Mhe. Susan Anselm Lyimo alisema uchaguzi wa Serikali za Mitaa Wabunge watawezaje kupata haki ya kupiga kura wakati mpaka mwisho wa uandikishwaji tarehe 29/11/2014 watakuwa Dodoma.

7. Mhe. Ester Amos Bulaya alisema Mahakama inatumika vibaya, Bunge lijadili na kila mmoja abebe mzigo wake.

8. Mhe. Mch.Peter Msigwa aliulizia kuhusu *Briefing* kwamba itafanyika lini kwani kuna malalamiko mengi ya wabunge na safari hii haikuwepo ni lini itafanyika?

9. Mhe. Joshua Samwel Nassari alisema wabunge wasijadili vyama bali taarifa ili wahusika wawajibishwe.

10. Mhe. Meshack Opulukwa aliulizia kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa kuhusu mihuri kuchaguliwa na CCM kwani wagombea wa vyama vingine wamewekewa zuio kwamba mihuri ya vyama vyao sio na wana CCM.

11. Mhe. Michael Lekule Laizer alisema Spika alisema Bunge linaendelelea na kuhoji kwani kumetokea nini Order Paper isifuatwe?

    Kiti kilieleza Bunge halijapokea Barua ya Zuio hivyo Bunge litaendelea na miongozo mingine itajibiwa wakati mwafaka.

## V. KUSITISHA BUNGE

Saa 6.00 Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni.

## VI. BUNGE KURUDIA

Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia likiongwa na Mhe. Spika.

## VII. HOJA ZA SERIKALI

Kabla ya Mwenyekiti wa Kamati kutoa taarifa ya Kamati yake ya PAC, Waziri wa Katiba na Sheria alitoa maelezo kuhusu zuizo la Mahakama kwamba Bunge kujadili suala la ESCROW na Spika naye alitoa maelezo ya ziada na kuomba Wabunge watumie nafasi hii kujadili hoja na sio watu binafsi na uchangiaji usiwe wa kulipiza kisasi au kwa kutaka urais mwaka 2015.

- Baada ya Hapo Mhe. Kabwe Zubeir Zitto, Mwenyekiti wa Kamati ya PAC alisoma Taarifa maalum ya Ukaguzi kuhusiana na miamala iliyofanyika

katika akaunti ya ESCROW ya Tegeta pamoja na umiliki wa kampuni ya IPTL.

- Mhe. Deo Haule Filikunjombe, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya PAC alimalizia kusoma Mapendekezo ya Kamati ambaye alitoa hoja na kuafikiwa na baadhi ya wabunge.

- Spika alitoa maelezo kwamba taarifa hii itaanza kujadiliwa kesho baada ya Serikali kutoa majibu ya maelezo yaliyotolewa na Kamati.

## VIII. KUAHIRISHA BUNGE

Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka tarehe 27/11/2014.

**DODOMA**
**26 NOVEMBA, 2014**

**DKT. T.D. KASHILILAH**
**KATIBU WA BUNGE**